

Ubatizo wa Watoto Wachanga

Kanisa ni Mama na Mwalimu

Wazazi kadhaa wameomba Ubatizo wa Watoto wachanga, utakaoadhimishwa mwezi huu katika makanisa madogo mbalimbali, kabla hatujingia katika kipindi cha Kwaresima.

Ubatizo wa Watoto wachanga huonyesha wazi kwamba Kanisa ni Mama wa watoto wa Mungu wengi. Funzo la Kanisa lasema kwamba ni vema kuwabatiza “kitambo kidogo tu baada ya kuzaliwa” (Katekismu, 1250). Tendo hili ni mapokeo ya Kanisa ya tangu karne ya pili, na ishara yake yapatikana hata katika Biblia (k.m. Mdo 16:15,33; 18:8). Kwa njia hii, watoto wetu waliopewa kipaji cha uhai, hujaliwa pia Uzima wa Wana wa Mungu na kukaribishwa katika Kanisa la Kristu. Pia, baadaye wataelimishwa katika imani ya Kanisa.

HABARI FUPI - HABARI FUPI - HABARI FUPI - HABARI FUPI

Associations & Groups

- YOUTH: Patrons Wapya na Kazi za Mwaka Mpya.

Kabla ya Noeli Patrons wawili wapya waliteuliwa na Parokia kwa ajili ya kikundi cha Vijana. Hawa ni bw. Peterson Muthua na bw. Anthony Nguni. Wakisaidiana nao, Vijana walianza kupanga kazi mbalimbali za mwaka huu. Januari walikutana kwa Semina katika Local Churches. Jumapili iliyopita, 2 Februari, walikuwa na sherehe ya Mtakatifu Yohane Bosko, Msimamizi wa Vijana duniani kote. Walikutana vikundi viwili: Dam Samaki (Mt. Karolo Lwanga Zone), na Gathanji Agroforestry (Mt. Maria Goretti Zone).

- CMA

Wanachama wa CMA wanaelekea kuchagua Viongozi wao. Jumapili 16 Februari kutakuwa na Uchaguzi katika kila Local Church. Kesho yake, Jumatatu 17 Februari, Viongozi watachoaguliwa watakusanyika Ol Moran, saa nne, ili kuwacha-gua Viongozi wa Parokia. Siku ya mwisho wa kujiandikisha kwa Chama ni Ijumaa 28 Februari.

- CWA

Jumatano 19 Februari, Executive Committee ya CWA itambelelea kanisa la Mithuri, saa nne asubuhi. Alhamisi 20 Februari, Ol Moran, saa tatu asubuhi, Wanachama wote watakutana kwa ibada ya Misa itakayoon-gozwa na Fr. David.

Siku ya mwisho wa kujiandikisha kwa Chama ni Ijumaa 28 Februari.

- CA

Jumatano 19 Februari, wanachama wa CA watatemelea kanisa la Ol Moran, saa nne asubuhi.

- CHOIR

Kutakuwa na Semina ya wanakwaya wa Parokia nzima Jumamosi 8 Februari, Kabati, kuanzia saa nne.

- SCOUT “Ol Moran 1”

Baada ya likizo ya mwezi wa Desemba, Maskauti walianza kukutana na kupanga kazi za Mwaka huu. Rovers na Mwamba watakuwa na safari kwenda Nyeri, Jumamosi 22 na Jumapili 23 Februari, ili kujiunga na Maskauti wa nchi na dunia watako-hudhuria sikukuu ya kuzaliwa kwake Baden Powell, mwanzilishi wa shirika la Maskauti. Baada ya safari, watawapokea vijana wapya wanaoomba kujiunga na kikundi chao. Kuna mpango wa kuanza Scouting Movement kwa ajili ya watoto wadogo pia katika Tumaini Academy.

Uteuzi wa Makatekista na Masomo ya Junior Catechists

Mabadiliko machache katika uteuzi wa Makatekista yaliambuliwa na PPC Jumamosi 25 Januari: Katekista Basilio Ngugi (Mithuri), aliyekuwa akihudumia kanisa la Mbombo, ametumwa katika Kanisa la Kabati kama Katekista Mkuu. Katekista Simon Njoroge, kutoka Kabati, ametumwa katika Kanisa la Dam Mbili kama Katekista Mkuu. Katekista Patrick Lowasa alitumwa katika Kanisa la Mbombo kama Katekista Mkuu, pia atahudhuria masomo ya Junior Catechists. Makatekista wengine wapya wameanza kusaidia makanisa kadhaa: James Gichuki (Mithuri) kwa kanisa la Mbombo; Alice Gachau (Ol Moran) kwa kanisa la Ngare-Narok; Felician Nyambura (Kabati) kwa kanisa la Ol Moran na PMC; Mary Ndegwa (Kinamba) kwa kanisa la Ol Moran na PMC.

Tena, Masomo ya “Junior Catechists” yataanza hivi karibuni, ili wengine wajifunze jinsi ya kulihudumia Kanisa kama Makatekista.

Huduma ya Madaktari

Mwezi huu wa Februari, katika Zahanati ya Parokia, kutakuwa na Madaktari wa watoto na wa watu wazima. Huduma yao itafuata utaratibu huu: Jumamosi 8: St. Martin (Kinamba); Jumanne 11: Ol Moran Cath. Disp.; Jumatano 12: Milango Pry. Sch.; Alhamisi 13: Nagum Pry. Sch.; Ijumaa 14: Kahuho Pry. Sch.; Jumamosi 15: Ol Moran Cath. Disp.; Jumatatu 17: Mouarak; Jumanne 18: Ol Moran Cath. Disp.

Sherehe ya kufungulia “Land of Hope”

Kituo cha Gallmann Memorial Foudation kinachoitwa “Land of Hope”, karibu na kijiji cha Mutaro, kitafunguliwa rasmi na “Maombi ya Matumaini” na sherehe Jumamosi 15 Februari 2014. Hapo kutakuwa na Shule ya Watoto (Nursery), kiwanja cha michezo na kazi nyingine za elimu na mazingira.

Kalenda ya Februari 2014

MAIN ACTIVITIES AND SUNDAY GOSPELS

Jumapili 9 Februari - ya 5 ya Mwaka - A - (Mt 5:13-16)

Jumanne 11 Februari - Siku ya Wagonjwa duniani kote

→ Ol Moran, 10.00am: Misa ya Wagonjwa

Jumamosi 15 Februari

→ Ol Moran, 10.00am: Mkutano wa Viongozi wa Mt. Karolo Lwanga

Jumapili 16 Februari - ya 6 ya Mwaka - A - (Mt 5:17-37)

Jumapili 23 Februari - ya 7 ya Mwaka - A - (Mt 5:38-48)

→ Ol Moran, 10.00am: Mkutano wa Viongozi wa Mt. Maria Goretti

Jumapili 2 Machi - ya 8 ya Mwaka - A - (Mt 6:24-34)

Jumatano 5 Machi - ya Majivu (Siku ya kufunga)

Mwanzo wa Kipindi cha Kwaresima

→ Mithuri, 11.00am: Misa na Ibada ya Majivu

→ Ol Moran, 3.00pm: Misa na Ibada ya Majivu

Ijumaa 7 Machi na kila Ijumaa ya Kwaresima:

Maombi ya Njia ya Msalaba katika makanisa madogo.

Jumapili 9 Machi - ya 1 ya Kwaresima - A - (Mt 4:1-11)

Harambee ya Parokia kwa ajili ya Ujenzi wa Kanisa

→ Ol Moran, 9.00am: Misa; 10.30am: Sherehe ya Harambee

Aliaga dunia wakiwa na Imani ya Kristu: Clement Kinyua (Githima, 26/01)

SAUTI YA MTAKATIFU MARKO

- No. 51, Year 6, Printed for private use at Ol Moran, Kenya, on 7th February 2014.

SAINT MARK CATHOLIC PARISH - Ol Moran - Catholic Diocese of Nyahururu
P.O.Box 20 - 20320 Kinamba - saintmark@olmoran.it - +254 720 924 153

Kwaresima na Paska 2014

Kipindi cha Kwaresima mwaka huu kitaanza tarehe 5 Machi, yaani Jumatano ya Majivu.

Kila Ijumaa, kama ilivyo desturi ya Kanisa, kutakuwa na Maombi ya Njia ya Msalaba katika makanisa madogo.

Pia, kila Jumapili ya Kwaresima, saa kumi, Ol Moran, yataadhimishwa Masifu ya Jioni: yaani kumsifu Mungu, kusikia Neno lake na kuabudu Ekaristi Takatifu.

Jumapili ya Matawi na mwanzo wa Juma Kuu itakuwa tarehe 13 Aprili. Sikukuu ya Paska ya Ufufuko itakuwa Jumapili 20 Aprili.

Harambee 2014

Askofu Luigi Paiaro na Wageni wengine

Askofu Luigi - Kamati ya Harambee ilimwalika Baba Askofu Mstaafu wa Nyahururu, Luigi Paiaro, kuwa mgeni wa heshima katika Harambee ya Jumapili 9 Machi 2014. Naye akakubali kwa furaha. Basi yeye atatuongoza katika ibada ya Jumapili, halafu atasimamia sherehe ya Harambee. Inafaa sana kwamba awe Askofu na rafiki yule ambaye atasimamia kazi hii ya Kanisa. Pia, kwa sababu ni mtu wa Kanisa, havezi kumzuia mgeni yeyote, awe mkubwa au mdogo, awe mwanasiasa au mfanyabiashara: wote wamekaribishwa kufika na kuuchangia ujenzi wa Kanisa.

Wageni wengine - Wageni wengi wengine walialikwa pia, na baadhi yao wameanza kuitikia: Viongozi wa Serikali, Wanasiasa au Wafanyabiashara. Majina yatatangazwa mara watakapohakikisha kuja kwao au msaada wao. Kutoka ng'ambo watakuja pia: Very Rev. Mons. Fausto Bonini (Venice); Rev. Fr. Silvano Bellomo (Paris); Arch. Stefano Battaglia (Venice).

Harambee 9 Machi 2014

PROGRAM

09.00am: Holy Mass

10.30am: Harambee Ceremony

CONTRIBUTIONS

M-Pesa: +254 720 924 153

(Parish Number registered under the name “Giacomo Basso”)

Cheques: Saint Mark Catholic Parish - Ol Moran

Bank Account: Cooperative Bank - Nyahururu: 01128038492900

Cash: At the Parish Administration Office or during Harambee Day

CONTACTS

P.O.Box 20 - 20320 Kinamba - KENYA

+254 720 924 153

saintmark@olmoran.it

SAUTI

YA MTAKATIFU MARKO



Gazeti la Parokia Katoliki ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran

N. 51 — Mwaka wa 6

Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia Alishi Yerusalem. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Halafu alishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Kwa hivyo, alikuwa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.

Januari-Februari 2014

Jumapili 9 Machi 2014, kwa ajili ya Ujenzi wa Kanisa Kuu la Parokia

Harambee!

Ujenzi wa Kanisa umeendelea sana, na wote sasa waweza kufahamu sura ya pekee ya mjengo huo. Hata hivyo, kazi bado ni nyingi, na hata gharama ya kumalizia si ndogo.

Tulianza kazi ya ujenzi Novemba 2012, tumeendelea na kazi mwaka wote 2013, na mwaka huu 2014 tunatarajia kumaliza kazi na kuanza kutumia kanisa letu.

Bila shaka, wakati wa kufungua kanisa utakapofika, tutafanya sherehe nzuri sana. Lakini, kwa sasa, wakati wa kupumzika haujafika: bado kazi ni kubwa na ni lazima kusukuma sote pamoja.

Nawashukuru Wakristu na marafiki walioshikamana kabisa mpaka saa hii. Sichoki kusema kwamba tuliyofaulu kufanya, yamewezekana kwa sababu ya kufanya kazi pamoja. Mchango wa pesa, mchango wa mahindi, sadaka nyingine, kazi za mikono, hayo yote tumeendelea kufanya. Mjengo huu hautakuwa kanisa tu, bali utakuwa hata ishara wazi ya nini watu wafaulu kufanya wakishikamana kabisa.

Tuna mwezi mmoja tu kabla ya Harambee. Kamati iliyoundwa kwa

ajili ya maandalizi ya sherehe ime-shakutana. Tujitahidi basi, na tujitolee hadi tuone matunda ya kazi yetu. Tutafute na kuwaita rafiki, watoto, ndugu na dada wa familia zetu. Wa-

pewe nafasi ya kuchangia na kubarikiwa kwa sababu ya tendo jema.

Kwa njia ya pekee namshukuru Askofu Mstaafu Luigi Paiaro aliyekubali kuja kama Mgeni wa Heshima. Kusema kweli, yeye kwetu si mgeni tu, ni Baba pia, rafiki na ndugu.

Nawaalika pia na kuwakaribisha sana wale wageni ambao watafika siku ya Harambee na kujiunga nasi katika bidii ya kutimiza ndoto na kazi yetu. Mbarikiwe kwa ukarimu wenu na urafiki wenu!

Fr. Giacomo Basso - Baba Paroko

Saint Mark Catholic Church at Ol Moran under Construction — January 2014



Fr. David Kinyanjui atakwenda kama Mmishionari kwa niaba ya Nyahururu

Kueneza Injili Marsabit

Ataondoka Ol Moran baada ya kuhudumia Parokia yetu kwa miaka karibu miwili. Fr. David Kinyanjui anatumwa kusaidia Jimbo la Marsabit, Kenya Kaskazini.

Mwezi wa Januari aliambiwa na Baba Askofu kwamba anatumwa kusaidia Jimbo la Marsabit kama Mmishionari kwa niaba ya Jimbo la Nyahururu. Kwa hiyo, Jumamosi 1 Februari, katika Misa ya Watawa wote wa Nyahururu, Askofu Joseph Mbatia alimpatia rasmi jukumu hilo.

Fr. David alikuja katika Parokia ya Ol Moran Machi 2012. Akisaidiana na Fr. Giacomo na Fr. Sebastian katika kazi zote za Parokia, alifuatilia kwa njia ya pekee hasa vyama (CA, CMA, CWA), Kwaya na Jumuiya Ndogo Ndogo.

Jumapili 9 Februari, Fr. David ataongoza ibada ya Misa Ol Moran, saa tano, halafu kutakuwa na sherehe ya kuagana naye. Baadaye atabaki bado siku kadhaa Ol Moran, ataondoka tarehe 21 Februari, atakaposindikizwa na Mapadri wengine kule Marsabit. Kwa njia hii, Nyahururu imeanza kazi ya Uenezaji wa Injili hata nje ya mipaka yake.

Tulimwuliza Fr. David maswali ili tujue zaidi lengo la jukumu lake.

Fr. David, kwa nini umetumwa Marsabit ingawa wewe ni Padri wa Jimbo la Nyahururu?

Ni kwa sababu ya mahitaji makubwa ya Jimbo la Marsabit. Ni jimbo lenye eneo kubwa sana, lakini lina Mapadri wachache bado. Kuna Parokia nane, lakini mbali sana moja kwa nyingine. Askofu Peter Kihara aliwaomba Maaskofu wengine wa Kenya wamsaidie na Mapadri. Kwenye Jimbo la Nyahururu, Askofu Jo-

seph aliwauliza Mapadri nani anaweza kujitolea kwa kazi hiyo. Siku moja mimi nilimwambia Askofu Joseph kwamba naweza kujitolea. Ulikuwa bado mwaka uliopita mwezi wa tano, hata muda ukipita nikasahau jambo hili. Tena, hata Mapadri wengine walikuwa wamekubali. Kumbé, baadaye Askofu akaniteua mimi, na mwezi wa kwanza akaniambia wakati umefika, afadhali nijandae kuondoka!

Umejua tayari mahali utakapokwenda, tena utakaa na nani, na utawahudumia watu wapi?

Kwanza, kwa muda nitakaa pamoja na Askofu kule mjini Marsabit. Baadaye yeye ataamua nitakapokwenda. Jimboni Marsabit watu ni hasa wa jumuiya ya Rendille, Borana, Gabra na Somali. Wengi wao wamo mwanzoni mwa Ukristu. Kazi yangu itakuwa ya Uenezaji wa Kwanza wa Injili. Lakini kwangu hicho si kitu kigeni, ni jambo nililojifunza hasa hapa Ol Moran, kwenye sehemu ya Kaskazini ya Parokia!

Umekaaje Ol Moran? Unawaachia Wakristu ujumbe gani?

Nimefurahia kuka hapa, na kwa kweli nina moyo mzito kuondoka. Nawaambia Wakristu wasaidie Mapadri katika Uenezaji wa Injili. Wawe watendakazi bora wa Injili. Wasirudi nyuma. Fr. James ataachwa peke yake kwa muda: jambo hili liwe changamoto kwao ili wajitolee na kutia bidii katika kazi ya Kanisa.

Hata hivyo, nitakuwa nikiwapitia. Njia ya kwenda Marsabit yapita Ol Moran! Urafiki wetu utaendelea. Bila shaka, tutasaidiana: ninyi mtanisaidia mimi, nami nitawasaidia ninyi.

Nawabariki na kuwapenda sana!

St. John XXIII Zone

Imepitishwa na PPC kwamba Mt. Karolo Lwanga Zone igawiwe mara mbili na kutengeneza "Zone" mpya inayohusu makanisa yaliyo katika sehemu ya Kaskazini, ambapo Parokia inafanya kazi ya Uenezaji wa Kwanza wa Injili (yaani 'First Evangelization'). Makanisa hayo ni: Nagum, Dam Mbili, Ol Donyo Ariwo, Kanjul na Lounyek.

Sehemu hiyo itaitwa "Mtakatifu Yohane wa 23 Papa" (St. John XXIII Pope). John XXIII alikuwa Baba Mtakatifu miaka 1958-1963, na atatangazwa kuwa Mtakatifu 27 Aprili 2014, pamoja na Papa John Paul II. Habari za maisha yake zasomwa katika The Echo.

PPC, PFC na Kamati ya Harambee

Mkutano wa PPC

Kulikuwa na mkutano wa PPC (Parish Pastoral Council), PFC (Parish Finance Council) na Kamati ya Harambee pamoja Jumamosi 25 Januari 2014.

Viongozi walikutana pamoja ili kujadiliana zaidi kuhusu mpango wa Harambee ya mwezi wa tatu, kuamua kazi iliyo lazima kufanya na kusoma ripoti ya michango iliyofanywa hadi sasa.

Walijadiliana kuhusu mambo mengine pia:

- Walikagua maendeleo ya mafunzo ya Katekismu kwa ajili ya Wakatekumeni, maandalizi ya Ubatizo wa Watoto Wachanga na kazi za Makatekista (tazama uk. 4 pia).
- Waliongea kuhusu kazi ya Uenezaji wa Injili katika sehemu ya Kaskazini ya Parokia, iliyokabidhiwa kwa ulinzi wa Mt. Yohane wa 23.
- Walipitisha Utaratibu mpya wa Ibadu za Mazishi ya Waumini Marehemu Wakatoliki. Utaratibu huo utatumwa katika makanisa madogo.
- Walipokea ripoti ya kazi za Vikundi na Vyama.

Hata Fr. Sebastian atakuwa nje ya Parokia kwa muda

Tukingoja Padri mpya katika Parokia

Kuanzia mwezi huu wa pili, hata Fr. Sebastian Gathogo atakuwa nje ya Parokia, lakini kwake siyo kuhamishwa. Bali, amepewa muda wa kupumzika na kusoma kwa miezi mitatu au mine, halafu atarudi. Askofu Joseph ametuahidia tayari kwamba atamtuma Padri mwingine Ol Moran badala ya Fr. David, lakini siyo mara moja: lazima kungoja hadi mwezi wa nne. Katika Parokia, basi, kutakuwa na upungufu wa huduma ya Mapadri kwa muda. Jumatatu 3 Februari, Baba Paroko alikutana na waakilishi wa Viongozi wa Parokia na Wafanyakazi ili kujadiliana nao kuhusu mpango wa kazi za Parokia kwa wakati huo. Kutakuwa na mabadiliko katika Utaratibu wa Misa za Jumapili na za Jumuiya. Hata mpango wa Baraka ya Familia zetu umeahirishwa. Lakini kazi nyingi lazima ziendeleo kama kawaida, viongozi wote wakishikamana zaidi.



Ziara ya Gavana wa Laikipia County

Irungu atembelea eneo la Ol Moran

Gavana wa Kaunti ya Laikipia, bw. Joshua Irungu, alitembelea eneo la Ol Moran Ijumaa 17 na Jumamosi 18 Januari, akiwa mgeni kwenye Parokia ya Ol Moran. Lengo la ziara yake lilikuwa hasa kujua miradi ya shule mpya za eneo na kuwatembelea wanafunzi. Alipata nafasi ya kuona hata shule na miradi mingine, na kukutana na viongozi wa Ol Moran. Ziara hiyo ilipangwa pamoja na Wachungaji wa makanisa mbalimbali, waliokuwa wamemwalika Gavana aje kuona yeye mwenyewe hali ya hizo shule na miradi mingine ya eneo. Gavana aliandamana na viongozi wengine wa Kaunti: Waziri wa Elimu, bw. Akaale J.B., na Waziri wa Usalama, bi. Agnes Keshine. Viongozi wengine walikuwa bw. Jacob Ikoeli (Member of County Assembly), bw. Manzi (Assistant County Commissioner, Sipili), bw. Samuel Njuguna (Sub-County Administrator, Rumuruti), bi. Leah Wanjiru Ithondeka (County TSC Director). Katika safari yake, Gavana alitaka kusindikizwa na Mapadri pia, ili apate kujua kazi ambayo Parokia imeendeleza hasa kwa njia ya SSP kwa ajili ya shule. Mpango uliofuatwa ulikuwa na mambo mengi, tena mazuri:

Ijumaa 17 Januari

- 7.30am: Shule ya Upili ya Mithuri na Shule ya Upili ya Ol Moran;
- 8.30: Gavana na wageni wengine walikaribishwa katika Parokia na kukutana na Mapadri na Wachungaji.
- 9.00: Ziara katika Shule za Msingi: **Tumaini Academy** (Ngare-Narok), **Nagum, Dam Mbili, Ol Donyo Ariwo, Kanjul, Lounyek, Magadi**. Kwenye shule, Gavana aliongea na wanafunzi, walimu na wazazi. Akawaachia zawadi pia: mpira ya michezo, na viatu pia kwa niamba ya Shirika la Msalaba Mwekundu.
- 7.00pm: Kufika Ol Moran na Chakula cha Jioni pamoja na Mapadri, Wachungaji, Masista, Viongozi wa Parokia (PPC, PFC).
- 9.00pm: Mazungumzo na Maombi pamoja na Wanafunzi wa **Hekima House**.

Jumamosi 18 Januari

- 7.00am: Ibadu ya Misa pamoja na Wakristu na Wanafunzi
- 8.00: Chai pamoja na Masista
- 9.00: Kutembelea miradi ya **shamba la Parokia**, hasa ya miti ya matunda.
- 9.30: Bonde na miti ya **Ngoisusu, Dam Samaki**; Miradi ya **Maji ya Ol Moran**.
- 12.00: Mkutano na **Viongozi** wa Eneo.
- 3.00pm: **Baraza** kijijini Ol Moran.
- 6.00pm: Chakula cha jioni na kuondoka.

Ziara ilisaidia sana kujadiliana kuhusu mambo mengi yanayohusu maisha ya watu wa kwetu. Iliongewa sana kuhusu changamoto za shule mpya, *registration* yao, maendeleo ya mijengo, kuajiri walimu, upungufu wa vitabu na vifaa, hata shida ya maji. Katika mkutano wa viongozi, masuala mengine yalizingumzwa: haja ya kutengeneza barabara kuu na nyingine, mashamba, usalama, mazingira (hata maoni ya kutengeneza "Corridor" ya wanyama wa porini kutoka Nagum mpaka Mugie), na mengineyo.

Matarajio ya Parokia ni kwamba mengi ya haya yaweze kutimizwa kwa muda unaofaa, tena Serikali na Kanisa zishikamane zaidi kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu, katika haki na amani.

Miradi mpya wa SSP

Masomo ya ECDE

Mradi mpya unaoendelezwa na SSP (*School Support Program*) ya Parokia ni masomo kwa ajili ya Walimu wa Watoto wadogo (*Nursery Teachers*) yaani E.C.D.E. (*Early Childhood Development Education*).

Masomo yataanza Mwezi wa Aprili 2014 (Jumatatu 14, isipobadilishwa kwa sababu ya kalenda ya shule), na yatafanywa katika Nyumba ya Wanafunzi "Hekima House". Mwalimu aliye na jukumu la kupanga na kuongoza masomo haya ni bw. Peter Savai. Masomo yataendelea miezi ya likizo (Aprili, Agosti na Desemba), mpaka kuwawezesha watahiniwa kupata *Certificate* au *Diploma*.

Wanaotaka kupata masomo haya, waweza kuchukua barua ya kujandikisha katika Ofisi ya Parokia, kwa bw. Peterson Muthua.

Masomo ya Computer

Pia, kuanzia mwezi huu, kutakuwa na masomo ya Computer (*Computer Packages*) kwenye Hekima House, wazi kwa watu wote, saa za mchana. Taarifa zaidi ziulizwe katika Ofisi ya SSP, kwa bw. Peterson Muthua.

School Support Program Sponsorship

Kamati ya Mradi wa Ufadhili wa Shule (SSP) ilikutana Jumatano 22 Januari ili kukagua maombi ya wanafunzi ya kupata msaada kwa ajili ya kulipa karo ya Shule za Upili. Kamati ilifanya uchunguzi wake kulingana na uwezo wa SSP yenyewe, matokeo ya mtihani ya wanafunzi walioomba msaada (Marks 315) na hali ya familia zao. Kama kawaida, SSP inasaidia wanafunzi wa Shule ya Upili ya Mithuri, ya Ol Moran au wa Hekima House.

Barua zimetumwa kwa wanafunzi na kwa shule, ili kuwajulisha wale walioweza kupata ufadhili huu. Kwa wanafunzi wanaosaidiwa na mradi huo, SSP yachukua jukumu la kulipa karo ya shule au karo ya Hekima House peke yake. Gharama zingine ni za familia. Tena, ni lazima kila mwanafunzi alete karatasi ya Matokeo ya Shule mwishoni mwa kila mhula, ili bidii yake ikaguliwe.

Wanafunzi waliokubaliwa katika SSP mwaka huu ni 19. Katika Shule za Upili na Hekima House watakosaidiwa na SSP mwaka huu ni wanafunzi 130 kwa jumla.

Baadaya maamuzi hayo, Ofisi haiwezi kupokea maombi mengine, hadi mwaka ujao.

Hekima House 2014

Wanafunzi wa Hekima House wa kidato cha 2, 3 na 4 walirudi Jumatatu 6 Januari na kuanza shule tarehe 7.

Jumatano 22 Januari Kamati ya SSP iliwachagua hata wanafunzi wanaoomba kujiunga na Jumuiya ya Hekima. Waliokubaliwa wataingia Jumatatu 10 Januari. Hawa ni wanafunzi 34 (wasichana 20 na wavulana 14). Kwa jumla, mwaka huu wanafunzi wa Hekima House watakuwa 100 (wavulana 45, wasichana 55).

Tumaini Academy - Mwaka wa Pili

Hata Tumaini Academy ilianza Mwaka Mpya wa Shule, Jumatatu 6 Januari 2014. Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Parokia mwaka huu wameongezeka mpaka 224 na shule imelifikia darasa la sita. Kuna hata walimu wapya walioajiriwa kwa sababu ya madarasa mapya.

Wakati wa kujandikisha umekwisha, na masomo yanaendelea. Hata hivyo, katika Nursery kuna bado nafasi na watoto wengine wanaweza kukubaliwa kuingia.



Fr. David Kinyanjui, pamoja na Askofu Joseph, Fr. Giacomo na Fr. Sebastian, siku ya Sherehe ya Parokia ya mwaka uliopita, Jumapili 9 Juni